KENYA NATIONAL ASSESSMENT TESTS
Kenya Certificate of Primary Education

504

# – KISWAHILI –
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA
## 2020 – Saa 1 dakika 40

---

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini.)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha kuchagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.
3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali 1–50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**
**Katika kijitabu cha maswali:**

**21.** Onyesha sentensi yenye kielezi cha mahali.
A. Hukimbizana mara kwa mara.
B. Wanafunzi watafuzu mwakani.
C. Kambo alisafiri kwa gari.
D. Tulielekezwa pembezoni.

Jibu sahihi ni D.

**Katika karatasi ya majibu:**

**1** [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [C] [D] **21** [A] [B] [C] [—] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi D ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

RRP
Kes 65/Set

© Worldmedia, 2020. Haki zote zimehifadhiwa.

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi **1** mpaka **15**. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hap... ..bu lifaalo **zaidi** kati ya yale ulivopewa.*

__1__ maisha yetu ya kila siku, tunatumia lugha kwa njia moja __2__ nyingine tangu tuamk... ____ tulalapo. __4__ si wengi wetu tunaojishughulisha na kuchunguza kwa undani maana na wajibu ... maishani mwetu. Tunaichukulia kuwa __5__ kitu cha kimaumbile tu. __6__ tukitua kidogo na kujiul... ____ namna gani kama hatungekuwa na lugha, ndipo tunapoweza kuelewa __8__ ya lugha maishan...

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. Kwa | B. Katika | C. Kwenye | D. Kati ya |
| **2.** | A. au | B. na | C. hata | D. pia |
| **3.** | A. kisha | B. tena | C. ila | D. hadi |
| **4.** | A. Isitoshe | B. Kwa hivyo | C. Hata hivyo | D. Aidha |
| **5.** | A. ni | B. kama | C. sio | D. ndio |
| **6.** | A. Japo | B. Labda | C. Bali | D. Maadamu |
| **7.** | A. yangalikuwa | B. yatakuwa | C. yangekuwa | D. yangelikuwa |
| **8.** | A. sababu | B. dhima | C. haja | D. thamani |

Mengi yamesemwa kuhusu dawa za kulevya. Dawa __9__ athari kubwa kwa watumizi wake ____ zimepigwa marufuku, kungali kuna wale __11__. Watumizi wake ni wa __12__ mbalimbali. Baadhi ya dawa ... mbaya ni bangi, miraa na pombe. Watumizi __13__ maisha yao. Kuna kuharibika kwa viungo kama ... kuchomeka, __14__ akili na kuwa punguani, kusambaratika kwa familia na __15__ kifo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. hii ina | B. hizo zina | C. hiyo ina | D. hizi zina |
| **10.** | A. Isipokuwa | B. Ingawa | C. Aghalabu | D. Angalau |
| **11.** | A. wanaozitumia | B. wanazozitumia | C. wamezitumia | D. wanazitumia |
| **12.** | A. kabila | B. jamaa | C. matabaka | D. taifa |
| **13.** | A. huhatarishia | B. huhatarishiwa | C. huhatarisha | D. huhatarishika |
| **14.** | A. kuvurugwa | B. kuvurugika | C. kuvuruga | D. kuvurugana |
| **15.** | A. hatimaye | B. ghafla | C. baadaye | D. pengine |

© *Worldmedia, 2020. Haki zote zimehifadhiwa.*

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi.*

**16.** Ni sehemu ipi iliyo tofauti na zingine miongoni mwa sehemu hizi za mwili?
- A. shavu;
- B. taya;
- C. paji;
- D. utosi.

**17.** Chagua usemi wa taarifa wa: ''Sitathubutu kumpa pesa zangu.'' Ali alisema.
- A. Ali alisema kuwa sitathubutu kumpa pesa zangu.
- B. Ali alisema kuwa hatathubutu kumpa pesa zake.
- C. Ali alisema kuwa hangethubutu kumpa pesa zangu.
- D. Ali alisema kuwa hangethubutu kumpa pesa zake.

**18.** Jibu la kitendawili: Nimesimama mbali nyikani lakini naonekana ni:
- A. twiga;
- B. mlingoti;
- C. moto;
- D. ukungu.

**19.** Ni sentensi ipi ambayo **si** sahihi?
- A. Pua yake imetiwa kipini.
- B. Maji ilimwagika yote.
- C. Ndizi niliyoinunua ndiyo hiyo.
- D. Sabuni zetu zina mapovu mengi.

**20.** Chagua kirejeshi kifaacho kujazia pengo: Tumboni mli ____ shiba hamna taabu.
- A. mo
- B. po
- C. ko
- D. o

**21.** Bainisha matumizi ya neno iliyopigiwa mstari katika sentensi: Kusoma <u>kwingi</u> kunasaidia kupita mtihani.
- A. kivumishi cha pekee;
- B. kivumishi cha sifa;
- C. kivumishi cha idadi;
- D. kivumishi kionyeshi.

**22.** Chagua jawabu **lilile** sahihi.
- A. Kata ni kuvunja kwa kutumia nguvu.
- B. Kata ni kupeperusha vitu hewani.
- C. Kata ni kutopenda kufanya jambo kwa haraka.
- D. Kata ni kivaa cha kubebea mizigo kichwani.

**23.** Chagua uakifishi ufaao wa: Fatu alishangaa ha kumbe alikuwa mahututi
- A. Fatu alishangaa. Ha kumbe alikuwa mahututi!
- B. Fatu alishangaa "ha kumbe alikuwa mahututi!"
- C. Fatu alishangaa, "Ha! Kumbe alikuwa mahututi!"
- D. Fatu alishangaa ha! kumbe alikuwa mahututi!

**24.** "Kwa" imetumiwaje katika sentensi: Mheshimiwa alipokelewa kwa shangwe na hoihoi?
- A. Kuonyesha kumiliki.
- B. Kuonyesha kielezi.
- C. Kuonyesha hali.
- D. Kuonyesha matumizi.

**25.** Ni orodha ipi ya maneno iliyopangwa jinsi yanavyotokea katika kamusi?
- A. Siti, Sista, Sisi, Sitiri.
- B. Mamlaka, Mamia, Maliwazo, Mandhari.
- C. Ghulamu, Gruneti, Gluu, Gumzo.
- D. Urafiki, Uraia, Uvumbuzi, Uwaziri.

**26.** Kutokeza na kuendelea vizuri kwa haraka ni kwa chipuka kama uyoga. Kumpa mtu sifa asizostahili ni kwa:
- A. kumvika kilemba cha ukoka;
- B. kumchezea shere;
- C. kumbwagia zani;
- D. kumpiga vijembe.

**27.** Ni kundi lipi lenye viunganishi pekee?
- A. isipokuwa, zuri, safi, ingawa.
- B. lakini, vizuri, wima, ila.
- C. ovyo, na, huyu, hao.
- D. maadamu, lakini, ingawa, ila.

**28.** Shangazi, wifi, amu ni majina ya:
- A. makundi;
- B. dhahania;
- C. jamii;
- D. wingi.

**29.** Kukanusha kwa: 'Nyuni akijenga kiota huishi humo', ni:
- A. Nyuni ajengapo kiota hataishi humo.
- B. Nyuni akijenga kiota hataishi humo.
- C. Nyuni anapojenga kiota haishi humo.
- D. Nyuni asipojenga kiota haishi humo.

**30.** Udogo wa: 'Kofia hii itatosha mtoto mdogo', ni:
- A. Kikofia hiki kitatosha kitoto kidogo.
- B. Kikofia hiki kitatosha mtoto mdogo.
- C. Kofia hii itatosha kitoto kidogo.
- D. Kofia hii itatosha toto dogo.

© Worldmedia, 2020. Haki zote zimehifadhiwa.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Maktaba ya kibinafsi ni maktaba iliyotengenezwa kwa matumizi ya mtu mmoja. Maktaba hii hupatikana katika vyumba vyetu na ni mkusanyiko wa vitabu, magazeti na majarida ambayo tunapenda kusoma. Katika maktaba hii, vitabu hupangwa katika rafu moja, mbili au tatu ndogo. Kila mwanafunzi anastahili kujitengenezea maktaba ya kibinafsi chumbani mwake kwa minajili ya kuhifadhi habari na mambo anayoyasoma.

Maktaba ya nyumbani ni maktaba iliyotengenezwa kwa matumizi ya familia nzima. Maktaba hii hupatikana katika chumba cha kusomea na ni mkusanyiko wa vitabu, majarida, magazeti na majalada ambayo familia inapenda kuhifadhi na kusoma. Katika maktaba hii, vitabu hupangwa katika rafu tatu hadi sita za wastani. Majalada hupangwa katika kabati kwa sababu yanahifadhi mambo muhimu yanayohusu familia. Kabati hii hufungwa na funguo kuwekwa pahala salama kama vile katika chumba cha wazazi.

Maktaba ya darasa ni maktaba iliyotengenezwa kwa matumizi ya wanafunzi na walimu wa darasa husika pekee. Maktaba hii mara nyingi huwa ni kabati kubwa ambalo husimamishwa nyuma ya darasa. Maktaba hii huwa na vitabu vya masomo yote wanayosoma wanafunzi hao. Pia huwa na ramani, michoro na vifaa vinavyotumiwa na wanafunzi katika darasa hilo. Maktaba hii hufungwa na funguo kuwekwa na kiranja wa darasa.

Maktaba ya shule ni kubwa kuliko ile ya darasa. Maktaba hii huwa na vitabu vingi kwa matumizi ya shule nzima na hutengewa chumba maalum. Katika chumba hiki kuna mhudumu ambaye huitwa mkutubi. Mkutubi hupanga vitabu, majarida na magazeti katika rafu na kusimamia shughuli zote katika maktaba kama vile kuazima vitabu. Mkutubi huhakikisha kwamba hakuna kelele maktabani. Maktaba hii huwa na sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni pahali pa kusomea, kufanya utafiti na kuandika. Sehemu ya pili ni pahali pa marejeleo. Vitabu vinavyopatikana katika sehemu hii husomwa maktabani tu yaani haviwezi kuazimwa kwa matumizi ya nje ya maktaba. Sehemu ya tatu ni iliyotengewa majarida na magazeti. Hapa pia wanafunzi hawaruhusiwi kuazima kwa matumizi ya nje ya maktaba.

Maktaba ya kitaifa ina sehemu tatu kama ile ya shule ijapokuwa ni kubwa zaidi kuliko ile ya shule. Hii ni kwa sababu inahudumia watu wengi: nchi nzima. Maktaba hii huwa na vitabu vya aina zote. Maktaba hii huwa katika jumba fulani lililotengwa kando na mengine, pahali patulivu pasipo shughuli nyingi. Ili kuomba kitabu, mtu huhitajika **kujisajili** kwanza na kupewa kadi maalum.

Kunayo aina nyingine ya maktaba ya kitaifa inayoitwa maktaba inayosafiri. Katika maktaba hii, vitabu hupangwa katika rafu katika gari kubwa na kusafirishwa hadi pahali vinapohitajika. Katika sehemu ambako usafiri wa magari ni mgumu, wanyama kama ngamia na punda hutumiwa katika usafirishaji huu.

Maktaba ni muhimu kwako wewe mwanafunzi kwa sababu ni katika maktaba tu utapata vitabu ziada vya kusoma, utasoma magazeti na majarida. Katika kufanya hivyo, utapata ukwasi wa lugha na kujiendeleza katika masomo yako yote. Pia utapata kujua matukio ya kila siku nchini mwako na ulimwengu mzima. Ni katika kusoma vitabu kama riwaya na ushairi, utapata hisia za kucheka au kulia kisha mshawasha wa kusoma zaidi na bila shaka **utakinaisha kiu yako**. **Usisahau kwamba kusoma hufanya akili ya binadamu kuwa katika hali ya hadhari**.

*© Worldmedia, 2020. Haki zote zimehifadhiwa.*

**31.** Maktaba inayopatikana mahali pengi nchini ni:
A. maktaba ya kitaifa;
B. maktaba ya shule;
C. maktaba ya nyumbani;
D. maktaba ya darasa.

**32.** Kulingana na kifungu, mkutubi hushughulika na mambo yafuatayo **ila**:
A. kupanga vitabu katika rafu;
B. kuandika vitabu mbalimbali;
C. kuazima vitabu;
D. kutuliza kelele maktabani.

**33.** Mwanafunzi anastahili kujitengenezea maktaba ya kibinafsi kwa madhumuni ya:
A. kuboresha matokeo shuleni;
B. kufuzu kama mkutubi;
C. kuhifadhi mambo anayoyasoma;
D. kuweka vifaa vinavyotumiwa nyumbani.

**34.** Kwa mujibu wa kifungu, vitu ambavyo hupatikana katika maktaba ya nyumbani ni:
A. vitabu, majarida na majalada;
B. magazeti, vitabu na ramani;
C. vitabu, ramani na michoro;
D. ramani, michoro na majarida.

**35.** Ngamia na punda hutumiwa katika shughuli za maktaba katika sehemu ambako:
A. usafiri wa magari ni mgumu;
B. vitabu havipatikani;
C. barabara hazipitiki;
D. kuna uhaba wa magari.

**36.** Kabati ambayo ni maktaba nyumbani na shuleni hufungwa ili:
A. kuzuia kuazimwa kwa vitabu;
B. kupunguza matumizi ya vitabu;
C. funguo ziwekwe pahala salama;
D. kuhifadhi vitabu visiharibike.

**37.** Maana ya "**kusajiliwa**" ni:
A. kufundishwa;
B. kuandikishwa;
C. kukaguliwa;
D. kunufaishwa.

**38.** Kwa mujibu wa taarifa, "**utakinaisha kiu yako**", inamaanisha:
A. utafurahia hali yako;
B. utapunguza tamaa yako;
C. utaongeza maarifa yako;
D. utatosheleza hamu yako.

**39.** "**Usisahau kwamba kusoma hufanya akili ya binadamu kuwa katika hali ya hadhari**."
Methali inayoweza kujumuisha maneno haya ni:
A. Mcheza kwao hutuzwa;
B. Udugu wa nazi hukutania chunguni;
C. Atangaye sana na jua hujua;
D. Chururu si ndo ndo ndo.

**40.** Chagua kichwa kifaacho **zaidi** kwa kifungu hiki.
A. Jinsi ya kuhifadhi vitabu;
B. Matumizi ya maktaba;
C. Aina za maktaba;
D. Umuhimu wa masomo.

© *Worldmedia, 2020. Haki zote zimehifadhiwa.*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Tipu alikuwa maarufu huko sehemu za kwao kutokana na kiburi chake. Lakini Waswahili husema **mgalla muue na haki umpe**. Licha ya kiburi chake hicho, Tipu alisifika kutokana na bidii zake za kujiendeleza kimaisha.

Tipu alikuwa mfanyabiashara katika soko la kwao, kazi aliyoianza baada ya kuuza maziwa kwa miaka mingi. Siku hizo alikuwa na mazoea ya kwenda kununua maziwa kwenye shamba la ushirika na kuzunguka kijijini akiyauza kwa baiskeli yake bila kuyajali maneno ya watu. Watu waliposikia kengele ya baiskeli walisema kwa sauti, "Haya, Tipu huyo na maziwa yake!" Hata hivyo wapo waliolalamika kuwa aliyatohoa maziwa yake kwa maji ili azidishe kipato chake. Lakini Tipu aliendelea na biashara yake. Biashara hii ilikuwa msingi mzuri wa kuishia kuanzisha kiduka chake cha kwanza. Muda si muda Tipu alipanda ngazi na kuwa na duka kubwa na kipato chake kubadilika sana. Hakuwa tena yule Tipu anayeipiga malapa baiskeli yake kila siku kuchuuza maziwa, bali mtu mwenye kiburi kingi. Isitoshe, alianza tabia nyingine ya kuwanyang'anya **washitiri** waliokwenda dukani mwake hasa wale wazee na wasiokuwa na uwezo wa kujitetea kama wanawake na watoto. Watu walichukia sana tabia hii na hata kupiga ripoti kwa chifu wa eneo hilo lakini hakuna lililofanyika. Tipu alikuwa na pesa za kutosha kumlainisha chifu huyo ili asichukue hatua yoyote au kumsema vibaya katika mikutano yake. Tipu akawa anajigamba kila wakati, "Nani alisema kuna kitu chenye uwezo mkubwa kuliko pesa ulimwenguni huu?"

Watu waliomjua tangu zamani waliifufua historia yake na kusema kuwa Tipu alifukuzwa shuleni akiwa kidato cha pili kutokana na wizi. Huo ndio uliokuwa mwisho wa elimu yake na mwanzo wa biashara yake ya maziwa. Wanakijiji waliendelea kuvilaani vitendo vyake huku naye akiyaendeleza matendo yake pamoja na unyang'anyi mkubwa.

Tabia ya Tipu ilifikia kilele wakati chifu wa eneo la kwao alipostaafu na Tipu mwenyewe kuteuliwa kuichukua nafasi yake. Zilikuwako tetesi kuwa alikuwa na jamaa fulani mwenye madaraka makubwa serikalini aliyehakikisha kuwa ameteuliwa kuitwaa nafasi hiyo. Tipu hakubadilika kamwe baada ya kukitwaa cheo cha uchifu; badala yake alikitumia cheo hicho kujitajirisha zaidi. Alihakikisha kuwa kila alipotaka kuweko na baraza, taarifa za baraza hizo hazikuenezwa vizuri. Hii ilikuwa mbinu yake ya kuhakikisha mahudhurio yenyewe yalikuwa mabaya na kwa hivyo kumpa sababu ya kuwatuma askari wake kwenda kuzisomba mali za watu kufidia 'kutohudhuria' mabaraza ya chifu.

Watu wa kwao waliendelea kulalamika lakini hayo **hayakumpiga mshipa** Tipu. Kila mara watu walipomwuliza, "Chifu Tipu, mbona unawanyanyasa watu na kuchukua mali zao?" yeye alijibu, "Hii sio mali ya watu, hii ni mali ya umma!" Wakati ukame ulipovamia eneo hilo na serikali kutuma msaada wa chakula, Tipu aliyachukua magunia yote na kuyatia kwenye maduka yake. Sasa tayari alikuwa na maduka mawili. Watu walilazimika kukinunua chakula hicho kutoka humo madukani mwake kwa bei ya juu. Kila alipoulizwa kisa na maana ya unyama huo, Tipu alisema tu, "Hiki si chakula cha mtu; hii ni mali ya umma!"

Hali iliendelea hivi hadi siku moja taarifa ya matendo ya Tipu ilipowafikia wakuu wake wa kazi. Wakati huo yule jamaa aliyemtegemea alikuwa amestaafu lakini Tipu aliamini hakumhitaji tena. Alikuwa ameshazoea unyang'anyi wake na hadi kudai hadharani kuwa ndege mkubwa hakamatwi kwa makapi. Wakuu wake kazini walifanya uchunguzi wao baada ya kukipokea kilio cha watu wa eneo hilo. Siku moja walifika makachero kwenye duka lake na kushuhudia Tipu akiwapunja wateja wake.

Tipu alitiwa pingu na kuchukuliwa na makachero hao. Wanakijiji walipomwona akiingizwa kwenye gari la polisi, walipaaza sauti, "Chifu Tipu, **je sasa umekwenda kula mali ya umma zaidi**?" Kijana mmoja alisema kwa sauti, "Jela kuna maharagwe na mahidi; hiyo Tipu ndiyo mali ya umma halisi. Nenda ukaifurahie kabisa!" Watu waliokuwa pale waliangua kicheko kikubwa licha ya uchungu waliokuwa nao kutokana na vitendo vya chifu wao.

Baadaye Tipu alifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la ufisadi na akafungwa jela kwa kipindi cha miaka mitano. Kijijini kisa chake kiligeuka wimbo wa kuwakumbusha watu matokeo ya ufisadi na kutumia madaraka yao vibaya.

Baada ya Tipu kupata makao mapya huko gerezani, maendeleo mengi yalianza kupatikana pale kijijini na kuifanya sehemu hii kuwa miongoni mwa baadhi ya maeneo yaliyoendelea zaidi kote wilayani.

*© Worldmedia, 2020. Haki zote zimehifadhiwa.*

**41.** Methali "**mgalla muue na haki umpe**" inahusianaje na maisha ya hapo awali ya Tipu?
- A. ingawa alikuwa na kiburi alikuwa na bidii za kazi.
- B. alikuwa maarufu licha ya tamaa yake.
- C. ingawa alifukuzwa shuleni aliteuliwa kuwa chifu.
- D. alijiendeleza kimaisha bila kuyajali maneno ya watu.

**42.** Kifungu kinaonyesha kwamba baada ya kuanza kupata utajiri, tabia za Tipu zilibadilika. Ni maovu gani aliyoanza kuwatendea watu?
- A. kuyatohoa maziwa kwa maji.
- B. kuwapunja wanawake na watoto.
- C. kuwauzia watu maziwa kwa bei ya juu.
- D. kulazimisha watu kuhudhuria mabaraza yake.

**43.** Tipu hakuchukuliwa hatua na chifu kwa sababu:
- A. alisifika katika sehemu za kwao.
- B. alimhonga chifu huyo.
- C. alikuwa mwenye uwezo mkubwa.
- D. alikuwa mwandani wa chifu huyo.

**44.** Maana ya '**washitiri**' kulingana na kifungu ni:
- A. wanakijiji.
- B. wanyonge.
- C. wateja.
- D. wenyeji.

**45.** Tipu alizidisha unyonyaji wake baada ya kutwaa cheo cha uchifu kwa:
- A. kumlainisha chifu aliyemtangulia ili asimseme vibaya kwa watu.
- B. kutumia cheo cha uchifu kujitajirisha kwa kuwadanganya wanakijiji.
- C. kuhakikisha kuwa mikutano yake haikutangazwa vyema ili walioikosa waishie kunyang'anywa mali yao.
- D. kuhakikisha kuwa taarifa za mabaraza yake zimeenezwa ili watu waweze kufidia mabaraza hayo.

**46.** Ni jibu lipi **lisilo sahihi** kuelezea maana ya '**mali ya umma**'?
- A. Mali inayopasa kufaidi nchi nzima.
- B. Mali inayomilikiwa na wananchi.
- C. Mali na rasilimali ya watu.
- D. Mali inayopasa kuwafaidi raia wote.

**47.** Kauli, "**je sasa umekwenda kula mali ya umma zaidi**" imetumia tamathali gani ya usemi?
- A. sitiari.
- B. tashihisi.
- C. utani.
- D. kinaya.

**48.** Kwa mujibu wa kifungu, mfuatano wa matokeo ufaao kuelezea ilivyokuwa hadi Tipu akaishia kifungoni ni:
- A. kilio cha watu kiliwafikia wakubwa wake, makachero walishuhudia akiwapunja watu, walitumwa makachero, alishikwa na kutiwa ndani.
- B. kilio cha watu kiliwafikia wakubwa wake, walitumwa makachero, makachero walishuhudia akiwapunja watu, alishikwa na kutiwa ndani.
- C. walitumwa makachero, makachero walishuhudia akiwapunja watu, kilio cha watu kiliwafikia wakubwa wake, alishikwa na kutiwa ndani.
- D. makachero walishuhudia akiwapunja watu, kilio cha watu kiliwafikia wakubwa wake, walitumwa makachero, alishikwa na kutiwa ndani.

**49.** Kwa mujibu wa kifungu, '**hayakumpiga mshipa**', ina maana:
- A. hayakumjalisha.
- B. hayakumkasirisha.
- C. hayakumsumbua.
- D. hayakumhangaisha.

**50.** Kulingana na kifungu, mafunzo yafuatayo yanajitokeza **ila**:
- A. umuhimu wa kuwajibika kazini.
- B. umuhimu wa kutunza dhamana tulizopewa.
- C. hatuwezi kufanikiwa maishani bila kupata elimu zaidi.
- D. hatupaswi kuyatumia madaraka yetu kujinufaisha.

*© Worldmedia, 2020. Haki zote zimehifadhiwa.*